# MWONGOZO WA KISIMA CHA MAARIFA KWA MWAKA WA MAFANIKIO 2020/2021

Karibu mwanamafanikio kwenye mwaka wetu mpya wa mafanikio 2020/2021.

Mwaka huu unaanza tarehe 01/11/2020 na kumalizika tarehe 31/10/2021.

Tumekuwa tunaanza mwaka wetu wa mafanikio mapema kabla ya wengine ili kujipanga vizuri na kuanza kuchukua hatua wakati wengine wanaenda kwenye mapumziko na kusubiri mwaka wa kawaida uishe.

Wanapokuja kuuanza mwaka mpya kwa hamasa ambazo hazidumu kwa muda mrefu, sisi tunakuwa tumeshapiga hatua kubwa zaidi.

## UTATU WA KISIMA CHA MAARIFA.

Kwenye KISIMA CHA MAARIFA tunaongozwa na utatu wa MSINGI, MWONGOZO NA MSIMAMO.

Msingi wetu ni NIDHAMU, UADILIFU NA KUJITUMA. Tunakuwa na nidhamu ya hali ya juu, tunakuwa waadilifu na kujituma kwenye kila tunachofanya.

Mwongozo wetu ni AFYA, UTAJIRI NA HEKIMA. Tunajenga na kuboresha afya yetu ya akili, mwili na roho, tunajijengea utajiri wa uhakika na kuwa wenye hekima kupitia kupata maarifa sahihi na kuchukua hatua.

Msimamo wetu ni KAZI, UPENDO NA HUDUMA. Rafiki yetu mkubwa na wa kwanza ni kazi, imani yetu kuu ni kwenye upendo na kwa kila tunalofanya ni kuwahudumia wengine.

Kwa utatu huu, maisha yetu yanakuwa bora na tulivu, tunakuwa na uhakika wa kufanya makubwa na kufanikiwa sana kwenye maisha yetu.

## IMANI KUU YA KISIMA CHA MAARIFA.

Kama wanachama wa KISIMA CHA MAARIFA tunaamini kwenye kitu kimoja ambacho ni UPENDO. Upendo ndiyo nguvu kubwa inayotuleta pamoja na kutuwezesha kufanya makubwa kwenye maisha yetu yenye manufaa kwetu na kwa wengine.

Katika kuishi imani hii ya upendo, tunazingatia mambo makubwa matatu;

Moja ni tunaanza kwa kujipenda sisi wenyewe, kwa kujitambua uimara na udhaifu wetu na kujikubali jinsi tulivyo. Hatujidharau wala kujinenea maneno mabaya. Tunajipenda na hivyo tunajilinda na kukazana kuwa bora zaidi.

Mbili ni tunawapenda wale wote wanaotuzunguka, tunatambua kwamba hatuwezi kufanya kitu chochote sisi wenyewe, mafanikio yetu yanatoka kwa wengine na hivyo tunawapenda watu wote wanaotuzunguka. Hatujengi uadui na mtu yeyote, tunawapenda wote bila ya kutegemea wanatupa nini. Kama kuna mtu ambaye hatupendi, hatumlipi kwa kutokumpenda, bali tunamlipa kwa kumpenda.

Tatu ni tunapenda kile tunachokifanya. Kazi na biashara ambazo tumechagua kuzifanya, tunazipenda kweli kweli, ndiyo kitu ambacho tumechagua kuweka umakini wetu wote. Hata kama siyo kitu tutakachokifanya milele, lakini wakati huu ambapo tunakifanya, tunakipenda. Tunaweka kila tulichonacho kwenye kazi na biashara zetu na hilo linatuweka kwenye nafasi ya kufanikiwa zaidi.

Kwa kujipenda wenyewe, kuwapenda wanaotuzunguka na kupenda tunachofanya, maisha yetu yanazungukwa na nguvu kubwa inayoleta kwetu kila tunachokitaka.

**AMRI KUU ZA KISIMA CHA MAARIFA.**

Mimi kama mwanachama wa KISIMA CHA MAARIFA ninayaendesha maisha yangu kwa kuzifuata amri hizi kuu;

1. Maisha yangu ni jukumu langu, kufanikiwa kwangu ni matokeo ya maarifa ninayopata na hatua ninazochukua.

2. Nitajipatia maarifa bora kila wakati na kuchukua hatua kwenye yale ninayojifunza. Nitasoma vitabu na kupata maarifa sahihi kwa njia nyingine zinazopatikana.

3. Kila wakati nitakazana kuongeza kipato changu zaidi kwa kutoa thamani zaidi kwa wengine kupitia kazi na biashara ninazofanya.

4. Kwenye kila kipato ninachoingiza, nitajilipa mwenyewe angalau asilimia 10 na kuiwekeza kwenye eneo ambalo linazalisha faida zaidi.

5. Nitakuwa mwanachama hai wa klabu ya KISIMA CHA MAARIFA iliyo kwenye mkoa wangu na nitashirikiana na wanachama wenzangu kutoa huduma mbalimbali kwa jamii inayotuzunguka.

6. Nitashiriki kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa KISIMA CHA MAARIFA ambapo napata nafasi ya kukutana na wanamafanikio wengine, kujifunza na kushirikishana nao mambo mazuri ya mafanikio.

7. Nitaishi kwa utatu wa KISIMA CHA MAARIFA siku zote za maisha yangu ambao ni #NidhamuUadilifuKujituma #AfyaUtajiriHekima na #KaziUpendoHuduma.

Nitazifuata amri hizi kwa kuwa zina manufaa kwangu na zitaweza kunipa kile ninachotaka kwenye maisha yangu.

**MPANGO TUNAOFANYIA KAZI KWENYE MWAKA WA MAFANIKIO 2020/2021.**

Kwenye mwaka huu mpya wa mafanikio 2020/2021 tunakwenda kuyaishi maisha yetu kwa utaratibu wetu wa KISIMA CHA MAARIFA ambao ni kufuata imani yetu, kwenda na utatu wetu na kuzisimamia amri zetu.

Lakini pia tutakuwa na vitu viwili vikubwa vya kufanyia kazi.

Kitu cha kwanza ni mpango wa MUONGO wa 2020 – 2030, kama nilivyoshirikisha na ambavyo tayari tumeshaanza, kila mmoja wetu ana mpango wake anaofanyia kazi kwenye muongo huu tuliopo sasa. Hili ni lengo kubwa ambalo mtu unataka kulifikia ndani ya miaka hii kumi tuliyopo sasa. Kila siku liandike lengo hili na chukua hatua kulifikia.

Kitu cha pili ni lengo la MWAKA WA MAFANIKIO 2020/2021 hapa unaweka mpango unaokwenda kufanyia kazi kwenye mwaka huu wa mafanikio. Weka lengo lako hilo na kila siku liandike na kuchukua hatua ili kulifikia.

Mambo hayo makubwa mawili utakuwa unayashirikisha kwenye tathmini za kila mwezi na kuonesha hatua ambazo umepiga kwenye kila eneo.

**KUWA KARIBU ZAIDI NA KOCHA.**

Kuanzia mwaka wa mafanikio 2020/2021 nimechagua kuwa karibu zaidi na kila mwanachama wa KISIMA CHA MAARIFA ili tuweze kusaidiana kupiga hatua zaidi kwenye maisha.

Kwa kipindi cha miaka 6 ambayo nimeendesha huduma hii ya KISIMA CHA MAARIFA, nimeifanya kuwa ya wazi ambapo mtu anaweza kujiunga na kuondoka wakati wowote anaojisikia, iwapo tu atakuwa amelipa ada.

Hilo limewakaribisha watu ambao hawajajitoa kweli kufanikiwa, nakazana kuweka juhudi kwao, hawafanyii kazi yale wanayojifunza na baadaye wanaondoka. Hilo limekuwa linanichosha sana kwa sababu juhudi kubwa ninazoweka sioni matunda yanayoendana nazo.

Kuanzia sasa nachagua kufanya kazi na watu wachache ambao wamejitoa kweli kufanikiwa, ambao wapo tayari kujifunza na kuchukua hatua na kunionesha hatua wanazochukua na matokeo wanayopata. Nataka kuwa karibu zaidi na watu hawa waliojitoa kweli, tuwe na mawasiliano ya karibu, nijue kila kinachoendelea kwenye maisha yao na wawe na nafasi ya kuwasiliana na mimi wakati wowote wanaponihitaji.

Kwa mpango huu mpya, nitakwenda kuwachuja sana wanachama waliopo sasa na hata wapya wanaokuja. Sitamlazimisha yeyote kwenda na mimi na nitataka kila mtu achague kama tunakwenda pamoja na asimamia uchaguzi huo aliofanya.

Nitakuwa tayari kutoa kila nilichonacho kwa wale waliojitoa kwa sababu najua wataweza kupiga hatua, bila kujali wanaanzia wapi.

Hivyo kama umejitoa kweli na unapanga kufanya makubwa kwenye muongo huu wa 2020 – 2030, karibu twende pamoja.

Kama ulikuwa kwenye KISIMA CHA MAARIFA kwa sababu tu unapenda kujifunza lakini haupo tayari kwa ukaribu huu wa kufanya kazi pamoja basi kutakuwa na njia nyingine nzuri kwako kuendelea kufanya hivyo, kupitia www.amkamtanzania.com na www.t.me/somavitabutanzania

Ukaribu mkubwa ninaokwenda kuutoa kwa wanachama waliojitoa kweli kufanikiwa ni kwenye maeneo yafuatayo;

1. Kutoa ushauri na mwongozo kwa hatua za mafanikio ambazo mtu anachukua.

2. Kusimamia kwa karibu (coaching) kwenye kila hatua.

3. Kutembelea eneo lako la biashara na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi ulionao.

4. Kusaidia kutengeneza mifumo mbalimbali kwenye biashara na shughuli nyingine unazofanya.

5. Kutumia kila kilicho ndani ya uwezo wangu, kukusaidia uweze kupiga hatua zaidi, kuanzia MAARIFA, UJUZI, KONEKSHENI na RASILIMALI kwa namna vinavyoweza kukusaidia.

Kama kweli umejitoa kufanikiwa na upo tayari twende pamoja kwa miaka hii kumi, karibu sana.

**NJIA KUU YA MAWASILIANO.**

Rafiki, njia kuu ya mawasiliano kwenye huduma hii ya KISIMA CHA MAARIFA ni barua pepe. Kwa kila mwanachama wa KISIMA CHA MAARIFA, utafungua uzi (thread) mmoja wa barua pepe ambao tutautumia kuwasiliana kwa mwaka mzima.

Kwenye uzi huo utaanza kwa kushirikisha malengo na mipango yako na kisha kila mwezi utatuma tathmini zako kupitia uzi huo mmoja.

Unapokuwa na jambo lolote unalotaka kuwasiliana na Kocha, unauliza moja kwa moja kwenye uzi huo. Kwa njia hii tutaweza kuona mawasiliano yetu yote ya mwaka mzima na pia yatakuwa na usiri mkubwa.

Unapokuwa na changamoto zozote au jambo unalotaka kumuuliza Kocha, unawasilisha kupitia email hiyo. Kocha atajibu na kama kuna haja ya mawasiliano ya simu au kukutana basi itapangwa.

**HATUA ZA KUCHUKUA.**

Hatua za kuchukua sasa ni hizi;

Ingia kwenye email yako na fungua kutuma email.

Kwenye TO (recipient) andika email; kochamakirita@gmail.com

Kwenye SUBJECT/TITTLE andika JINA LAKO MWAKA WA MAFANIKIO 2020/2021 (Mfano; MAKIRITA AMANI MWAKA WA MAFANIKIO 2020/2021)

Kwenye sehemu ya kuandika email jaza yafuatayo;

1. Majina yako kamili, mawasiliano yako ya simu na eneo unalopatikana na kufanyia shughuli zako (Mkoa, wilaya na mtaa/kijiji).

2. Taarifa zako kwa ufupi, tarehe, mwezi na mwaka wa kuzaliwa, jinsia, kabila, dini, kiwango chako cha elimu na hali yako ya kifamilia, kama una mume/mke na watoto wataje kwa majina yao.

3. Shughuli kuu unazofanya, iwe ni kazi ya kuajiriwa au kujiajiri na biashara unazofanya pamoja na uwekezaji.

4. Ndoto kuu ya maisha yako, ni kitu gani hasa unachotaka kufikia kwenye maisha yako, unajiona ukiwa wapi na maisha yako.

5. Mafanikio yana maana gani kwako, ni kigezo gani unachotumia kupima mafanikio yako, maisha yako yakiwaje ndiyo unajihesabu umefanikiwa.

6. Lengo kuu unalofanyia kazi kwenye muongo huu wa 2020 – 2030.

7. Lengo kuu unalofanyia kazi kwenye mwaka huu wa mafanikio 2020/2021.

8. Njia utakazotumia kujipima kila mwezi kwenye kufikia lengo kuu la mwaka na lengo kuu la muongo.

9. Changamoto kubwa ambazo zimekuwa kikwazo kwako kwa muda mrefu na unaona zitazidi kuwa kikwazo, pamoja na hatua ambazo umepanga kuchukua ili kukabiliana na changamoto hizo.

10. Ahadi yako ya kuwa mwanachama wa KISIMA CHA MAARIFA na kufuata miongozo yote ya mafanikio na kushirikiana na wengine ili kupiga hatua zaidi.

Rafiki, taarifa hizi ni nyingi na zinaingia ndani zaidi lakini jua zitakuwa siri baina yangu na wewe na sitazitoa kwa yeyote yule bila ruhusa yako. Hivyo jisikie huru kunieleza kwa uwazi, sitakuhukumu kwa lolote. Lengo ni nataka nikufahamu vizuri ili tuweze kushirikiana kwa mafanikio yetu wote.

Karibuni sana kwa wale ambao mmejitoa twende pamoja kwenye safari hii ya mafanikio.

Tuma taarifa hizi kama nilivyoelekeza kuanzia tarehe 08/11/2020 mpaka tarehe 14/11/2020.

**TATHMINI ZA KILA MWEZI.**

Utaratibu wetu wa tathmini za kila mwezi utaendelea na kila tarehe moja mpaka tarehe tano ya mwezi mpya unatuma tathmini ya mwezi uliomalizika.

Katika tathmini hizo za mwezi utajibu maswali yafuatayo;

1. Andika lengo kuu la muongo wa 2020/2030 na la mwaka wa mafanikio 2020/2021.

2. Eleza hatua ulizochukua kwa mwezi uliopita kwenye lengo la muongo na lengo la mwaka na matokeo uliyopata.

3. Andika kiasi cha kipato ulichoingiza kwa mwezi ulioisha, njia ulizotumia kuingiza kipato hicho, akiba uliyoweka na uwekezaji uliofanya.

4. Andika maarifa mapya uliyopata kwenye mwezi ulioisha kupitia vitabu na njia nyingine na hatua za tofauti ulizochukua kwa maarifa hayo.

5. Kama kuna changamoto yoyote umekutana nayo mwezi uliopita ieleze na hatua ulizochukua kuikabili.

6. Andika mpango unaokwenda kufanyia kazi mwezi huu mpya kwenye lengo la muongo na lengo la mwaka.

7. Kama kuna ushauri ambao ungependa kupata kutoka kwa Kocha karibu uulize. Na kama kuna ushauri uliupata kwa kocha na kuufanyia kazi, shirikisha matokeo uliyopata.

Tathmini zinatumwa kwenye uzi mmoja ambao umeuanzisha wa kuwasiliana na Kocha.

Niwakaribishe wote kwenye safari hii ya mafanikio, twende pamoja, tukishirikiana kwa karibu na tuweze kupiga hatua zaidi.

Rafiki yako,

Kocha Dr Makirita Amani.